

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 09 hadi 27 Machi, 2020 Jijini Dodoma. Kamati hizo zinakutana kabla ya Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 31 Machi, 2020. Shughuli zote za Kamati zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- a. Kupokea Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mpango, Kiwango na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Shughuli hii itafanyika tarehe 11 Machi, 2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) na (2).
- b. Kamati za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kisha kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.
- c. Kamati ya Bajeti itafanya uchambuzi wa Mapendekezo ya Serikali ya Mpango na Kiwango cha Bajeti kwa ajili ya kuzishauri Kamati za kisekta.
- d. Kamati ya Sheria Ndogo itafanya uchambuzi wa sheria ndogo mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge.

- e. Kamati za Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) zitafanya ziara za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwenye miradi mbalimbali nchini.
- f. Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji zitashughulikia miswada mitatu iliyosomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Nane.

Ratiba za Shughuli za Kamati za Bunge pamoja na maeneo ambayo Kamati hizo zitafanya ziara inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz.

Imetolewa na:- Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

06 Machi, 2020.